**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**Mtaa wa Urambo,**

**Simu Nambari: 2150043 – 6/2150360**

**11102 ILALA**

**Fax No: (022) 2150047**

**ILALA – JULAI 8, 2020**

# TAARIFA KWA UMMA

## UTENDAJI WA TAKUKURU MKOA WA ILALA KWA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI, 2020

**NDUGU WANAHABARI.**

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kuitikia wito wetu na kuja kushiriki kwenye mkutano huu. Karibuni sana ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala.

**NDUGU WANAHABARI.**

Ni utaratibu wetu TAKUKURU kutoa TAARIFA YA UTENDAJI KAZI kwa umma katika kipindi cha kila robo mwaka kupitia kwenu wanahabari. Leo TAKUKURU Mkoa wa Ilala tunatoa TAARIFA YA UTENDAJI KAZI kwa kipindi cha **Aprili hadi Juni, 2020**. Kama inavyofafanuliwa hapa :-

## 1.0. MAHAKAMANI

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala imefungua kesi mpya 05, na mashauri 22 yanaendelea Mahakamani kama ifuatavyo: Mamlaka ya Mapato (TRA) Mashauri 3, Serikali za

Mitaa mashauri 3, wafanyabiashara mashauri 2, idara ya afya mashauri 4, Ujenzi (TANROARDS) Shauri 1, Utapeli shauri 1, Elimu ya Juu Mashauri 2, Mahakama shauri 1, Taasisi za fedha shauri 1, vyama vya siasa shauri 3, Maji (DAWASA) shauri 1. Takukuru Mkoa wa Ilala pia imeshinda kesi 3.

## 2.0. UCHUNGUZI

Katika kipindi hicho pia TAKUKURU Mkoa wa Ilala tumepokea taarifa 157 katika taarifa hizo malalamiko yaliyohusu rushwa ni 72, ambapo taarifa 18 ni za polisi, 17 ni za serikali za Mitaa, Afya 04, Ardhi 07, Mahakama 09 na Elimu 07, uchunguzi wa taarifa hizi unaendelea katika hatua mbalimbali.

TAKUKURU Ilala inaendelea na uchunguzi wa tuhuma ya ubadhirifu wa fedha kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 1.6 uliofanywa na viongozi wa TALGWU SACCOS kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi 2017. Uchunguzi wa suala hili upo katika hatua za mwisho.

Pia TAKUKURU Ilala inafanyia kazi mgogoro wa Ardhi katika Mtaa wa Mbondole, Kata ya Msongola kuhusu ufufuaji wa mipaka ya viwanja vilivyotajwa kuwa ni vya walimu. TAKUKURU imeingilia kati suala hili ili haki iweze kutendeka kwa wananchi ambao wameporwa maeneo yao.

## 3.0. UELIMISHAJI UMMA.

Kama nilivyotangulia kusema kuwa tunalo jukumu la Uelimishaji Umma.

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 Dawati la Elimu kwa umma Mkoa wa Ilala tumeweza kuelimisha makundi mbalimbali kwa njia ya vipindi vya redio na TV, semina,mikutano ya hadhara, mikutano na waandishi wa habari, maonesho, uimarishaji na ufunguzi wa klabu katika shule za msingi, sekondari na vyuo.

*Katika kipindi cha Julai hadi Septemba tunajipanga kufanya mikutano ya hadhara zaidi kwa ajili ya kuwapa wananchi elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa katika uchaguzi kwani sote tunafahamu kuwa mwaka huu tuna zoezi la uchaguzi mkuu.*

## 4.0. UZUIAJI RUSHWA

Katika kuhakikisha kuwa kero mbalimbali zinapatiwa ufumbuzi, na wakati mwingine kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kupata njia sahihi ya kuishauri Serikali kuhusiana na masuala ya rushwa katika mkoa wetu tumefanikiwa kufanya yafuatayo:

i. Uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa mikopo isiyo na riba kwa wanawake , vijana na walemavu ili kubaini mianya ya rushwa katika mfumo wa utoaji na usimamizi wa mikopo husika na kuimarisha mfumo wa utoaji wa mikopo hiyo.

*Pamoja na kuchambua mfumo pia ofisi imefuatilia matumizi ya fedha za umma (PETS) kwenye miradi ifuatayo:-*

*i) Mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi kilichopo Mbezi Luis wenye gharama ya shilingi 50,947,589,580.20. katika ufuatiliaji wa mradi TAKUKURU imewezesha mradi kuendelea kwa kasi iliyokusudiwa na dosari mbalimbali zimeendelea kurekebishwa katika mradi.*

*ii) Ufuatiliaji wa mgawanyo na matumizi ya fedha za kampeni dhidi ya COVID -19 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, ambapo kwa kipindi cha Aprili- Juni 2020, jumla ya Tsh, 77,500,000.00 zilipokelewa kutoka UNICEF kwa ajili ya mradi wa WASH (Water Sanitation and Hygiene)*

Tunatekeleza jukumu hili kwa mujibu wa Kif cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 ambapo kupitia ukaguzi huu

tunajiridhisha iwapo kuna thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za serikali zinazotolewa kutekeleza miradi hiyo.

**KUELEKEA UCHAGUZI MKUU WA VIONGOZI**

**Ndugu wanahabari:**

Sote tunafahamu kuwa mwaka huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu. TAKUKURU (M) ILALA tuna jukumu la kufuatilia na kuhakikisha wagombea wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika mchakato wa uchaguzi tunawabaini. Hivyo tumejipanga kufuatilia mchakato mzima wa uchaguzi na kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa vitendo vya rushwa ndani ya mkoa wa Ilala vinadhibitiwa KABLA, WAKATI na BAADA ya Uchaguzi Mkuu.

**MWISHO**

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwenu waandishi wa habari kwa kukubali kuja kunisikiliza na hasa tukizingatia umuhimu wa shughuli yenu ya habari. Napenda kutoa wito kwenu kuendelea kutoa elimu juu ya adui rushwa kwa jamii. TAKUKURU inawaomba mkaendelee kuwa mabalozi madhubuti wa mapambano dhidi ya rushwa.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

**IMETOLEWA NA**

**Christopher Myava**

**KAMANDA WA TAKUKURU (M) ILALA**